**LEARNING BY EAR**

**“Mihadarati na vileo-poromoko la jamii”**

**Episode 3: “Mtego wa panya..”**

**Author: Chrispin Mwakideu**

**Editor: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo**

**Proofreader: Charlotte Collins**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: OUTSIDE CLUB 2000**

- **Jabali (m, 18)**
- **Zula (m, 18)**
- **Okosho (m, 18)**
- **Chambo (m, 30)**

**SCENE TWO: BERI AND PUYANGA AT HOME**

- **Puyanga (m, 50)**
- **Beri ( f, 45)**

**SCENE THREE: BEHIND CLUB 2000**

- **Jabali (m, 18)**
- **Zula (m, 18)**

- **Okosho (m, 18)**

**SCENE FOUR: PUYANGA AND BAMJU AT A CAFE**

- **Puyanga (m, 50)**
- **Bamju (m, 40)**

**SCENE FIVE: AT THE POLICE STATION**

- **Beri (f, 45)**
- **Inspector Tino (m, 40)**
- **Jabali (m, 18)**

**MSIMULIZI (m/f)**

**INTRO:**

Hamjamboni na karibuni katika kipindi chetu cha tatu cha, Noa bongo, jenga maisha yako. Tukiangazia matumizi ya mihadarati na vileo vyengine katika mchezo wa kuigiza uitwayo "**Poromoko la Jamii**"**.** Katika kipindi kilichopita kamishna wa polisi Beri alipigwa na butwaa alipoona dawa za kulevya katika droo ya mumewe, pamoja na maagizo ya mauzo makubwa ya mihadarati hiyo. Jabali alijaribu kutafuna miraa na rafiki zake_Okosho na Zula, lakini ikamshinda. Wakiwa bado nje ya kilabu, Okosho akavumbua njia ya kuwaingiza ndani bila vitambulisho. Swali ni kuwa, watafaulu? Hususan ikiwa Chambo yuko katika lango la kuingilia? Ni manusura wa mihadarati baada ya kutembelea kituo cha kurekebisha tabia, na amejitolea mhanga kupinga mihadarati na vileo vyengine. Endelea kusikiliza hatima ya hadithi hii katika kipindi cha leo kiitwacho, "**Mtego wa panya…**" Tunatabaruku na vijana hao watatu wakiwa na mjadala wa mpango wa kuingia kilabuni.

**SCENE ONE: OUTSIDE CLUB 2000**

1. **SFX: DJ music from outside**

2. **JABALI:** **(adamant)** La! Okosho, turudini nyumbani. Unaonekana mlevi, na Zula pia ashachanganyikiwa.

3. **OKOSHO:** Aste aste, Jabali. Shida iko wapi. Utamueleza kuwa wewe wasomea udaktari. Unafanana nao hata hivyo. **(giggles)** Zula na mimi tuko chuo cha ufundi. Tunajifunza useremala.

4. **ZULA:** Useremala? Hapana, mameni. Zula boy hawezi kuwa seremala! Mimi ni fundi wa magari! Tunasomea uhandisi wa magari. Wanipata nadhani.

5. **OKOSHO:** Haijalishi bwana. Twendeni; baridi imeanza kutanda. Na msisahau kuweka sura za ki utu uzima

6. **JABALI:** **(curious)** Ndio zikoje hizo sura?

7. **OKOSHO:** Tazama ishara zangu za nyuso! Onaona, sura ya mtu aliyekula chumvi iko hivi. Sawa, twendeni.

**(Zula na Okosho wanacheka)**

8. **SFX: MUSIC GETS BIT LOUDER, THEN SOFTER AS THEY BEGIN TO**

**TALK. FOOTSTEPS APPROACH**

9. **CHAMBO:** Ah, umerudi. Kama nilivyokwambia, naitwa Chambo, na ni mwanzilishi wakikundi cha Youth Watch, shirika la kibinafsi linalohusika na maswala ya jamii. Kuona kwamba vijana wetu wameepushwa na mihadarati. Niko hapa kutazama vitambulisho, kwa maana vilabu ni miongoni mwa sehemu nyingi ambamo vijana hujifunza kutumia mihadarati na vileo vyengine. Je muko na vitambulisho vyenu?

10. **OKOSHO:** **(faking excuse)** Aah …Chamba Wamba…

11. **CHAMBO:** Chambo, naitwa Chambo.

12. **OKOSHO:** Sawa… **(clears throat)** Chambo, sisi ni wageni hapa. Hawa ni rafiki zangu, na … tumeufanya ujinga sana… na tukasahau vitambulisho vyetu chuoni. Huyu ni Jabali, anasomea udaktari. Zula na mimi tuko chuo cha ufundi. Tunasomea useremala.

13. **ZULA:** Uhandisi.

14. **OKOSHO:** **(caught off guard)** Ah Ndio… Uhandisi-useremala!

15. **CHAMBO:** Nendeni nyumbani.

16. **OKOSHO:** Eti? Kwanini? Sisi ni…

**17. CHAMBO:** Nishasikia uongo kama huo, hata mimi nilidanganya sana. Na mnajuwa nini? Hamunifiki kuongopa. Najuwa mumebeba nini kwenye huo mfuko, na najuwa nyinyi wawili tayari muko chopi. Huyu, sijui. Lakini nawahusia muache kutumia vileo hivyo kabla havijawadhuru.

**18. ZULA:** Nani huyu anatusomea? Eh? Sisi si watoto! Tunaweza kufanya chochote, mamen! Ishia!

**19. JABALI:** Sikutarajia usiku wa namna hii. jamaa, tuachane na haya turudi nyumbani. Sawa?

**20. OKOSHO:** **(fuming)** Hapana! Hatuendi mahali! Huyu mjinga anafikiri anatujuwa. Kama ni mwanamume, njoo tukutane kiume!

**21. ZULA:** Ndio, njoo kule tuonane kiume. Tutakufunza kiume! Mamen!

**22. CHAMBO:** **(not threatened)** Nitakuwa napeana maongezi kuhusu mihadarati na vileo vyengine katika shule ya upili ya Limbi High adhuhuri ya kesho. Nawaalika. Kwaherini, na usiku mwema.

**23. ZULA:** Ni Bi. Chacha! Alitueleza kuhusu huyu mtu. Yule mchawi! Alijuwaje tunatoka shule ya upili ya Limbi?

**24. CHAMBO:** Aha, Sasa ninafahamu. Kwa hivyo nyinyi ni wanafunzi wa Limbi. Musihofu kitu. Nendeni nyumbani, na tafadhalini musikose kongamano hilo.

**25. OKOSHO:** Kwa taarifa yako, tulimaliza masomo ya shule ya upili ya Limbi! Hatutaki kusikia upuuzi wowote kutoka kwako, au kwa Bi. Chacha, au wa mjinga mwengine yeyote.

**26. JABALI:** Okosho, Zula – jamaa twendeni. Mumemsikia mnoko – hatuingii bila vitambulisho.

**27. CHAMBO:** Ni vyema kumsikiliza vile mwenzenu anavyosema. La sivyo itanibidi nimuite mlinzi, na hatakuwa na usuhuba na nyinyi.

**28. OKOSHO:** Wangoja nini! Muite. Ni rafiki yangu, hata hivyo.

**29. CHAMBO:** **(calls out)** Mlinzi! Mlinzi! Hebu njoo, tuna shida kidogo.

**30. JABALI:** Jamaa sio vizuri, Haifai jamaa kabisa.

**31. MSIMULIZI:** Jabali anasema kweli, kwa sababu mlinzi alipokuja alimshika shati Okosho, akambeba kama ambae ana uzito wa kilo moja na kumburura kutoka langoni, wakati Zula na Jabali wakimrai amsamehe. Vijana hao wawili watafanyaje? Kaa nasi ugundue. Kwa sasa, Kamishan wa polisi Beri alipopata ya kuyapata katika droo ya mumewe ilibidi akwishiwe na nguvu. Baada ya muda mchache, Puyanga alirudi nyumba.

**SCENE TWO: BERI AND PUYANGA'S HOME**

**32. BERI:** **(takes a very deep breath)** Sawa. Vile ambavyo nimeyapata haya, nichukuwe hatua kama mke wake, au kama afisa wa polisi?

**33. SFX: KNOCKING ON DOOR**

**34. BERI:** Oh, hapana… Amerudi!

**35. SFX: DRAWER CLOSED QUICKLY AND LOCKED**

**36. BERI:** **(calls out)** Naja! **(nervous whisper)** Nimeregesha kila kitu kilivyokuwa? Sawa- sasa imekbaki kitu kimoja…

**37. SFX: WATER BEING FLUSHED IN TOILET**

**38. BERI:** **(calls out)** Pole, mpenzi wangu, nilikuwa chooni. Nitakufungulia mlango.

**39. SFX: DOOR BEING UNLOCKED**

**40. PUYANGA:** **(drunk)** Umecheleweshwa na nini? Mmmh?

**41. BERI:** Nilikwambia, Nilikuwa msalani. Nataka unijibu: wewe watoka wapi?

**42. PUYANGA:** **(aggressive)** Tuyazungumze hayo kesho. Nimechoka.

43. **BERI:** Kesho? Haya hayatangoja kesho. Mumewangu…

44. **SFX: SOUND OF SLAP ON FACE**

45. **BERI:** **( screams in pain)** Owww!

46. **PUYANGA:** **(with emphasis)** Kesho, sawa? Sitaki maswali zaidi.

47. **MSIMULIZI:** Familia na wendani wengi hukataa kusadiki wanapogundua watu waliokaribu nao kuwa ni waathiriwa wa mihadarati. Hofu huwatanda, kutosadiki, hujihurumia, au kuongozwa na hisia tofauti.maswali chumbi chumbi yasiyo na majibu. Husambaratika zaidi wakati waasiriwa hao huanza kuwapiga, kuwaibia, na hata kuwatishia. Hata Beri, afisa wa polisi wa ngazi za juu, hakuepukwa. Atamkimbilia nani? Kwa sasa, nje ya kilabu 2000, Okosho na Zula bado wanang'ang'ania kujivinjari usiku huo.

**SCENE THREE: BEHIND CLUB 2000**

48. **SFX: MUSIC NOW PLAYING IN THE DISTANCE**

49. **OKOSHO:** Jinga! Yule mlinzi hatawahi kupata chochote tena kutoka kwangu! Nipe moshi, Zula, na fungua pombe. Hata kama hatutaingia kilabu ni lazima tujipe raha.

50. **ZULA:** Ama vipi, mamen!

51. **JABALI:** La, Zula, hapana njia ni kurudi nyumbani! Mbona tunajidhalilisha?

52. **SFX: CLANKING OF BOTTLES, MATCH BEING STRUCK (studio)**

53. **OKOSHO:** **(inhales deeply)** Ooooh… Nasikia raha ajab! Hiyo, Zula… pata moshi, alafu mpe msomi wetu.

54. **ZULA:** **(also inhales deeply, then exhales))** Mameni, bangi bangili, mamboye mawili! Wazimu au akili! Kwako, Jabali.

55. **JABALI:** La, asante. Usiku umenitosha.

56. **OKOSHO:** Mkupuo mmoja ukuburudishe. haitakusanifu. Hebu nitazame – si bado niko poa.

57. **ZULA:** Eeeh.. Mimi pia…

**58. JABALI:** **(hesitant)** Ah – Sawa. Bila shaka mara moja haitaleta tofauti... **(JABALI inhales, then coughs uncontrollably)**

**59. OKOSHO/ZULA: (laughing out loud)** Hahahahahaha!

**60. MSIMULIZI:** Kwa hivyo, kama ilivyokuwa, Jabali alikiakia chambo. Baada ya mkupuo mmoja, wa pili, wa tatu na mengine ikafuatia. Alikunywa pombe ambayo pia ilikuwa imechanganyiwa virangaona vyengine vya ulevi, na bila kujijuwa alikuwa tayari ametekwa na pombe. Badala ya usiku atakaoukumbuka sasa alikuwa katika usikuambao hakuujua ulipita vipi. Sasa, iwavyo, ni asubui iliyofuata, na mumewe Beri, Puyanga ana mkutano mgahawani – na jambazi Bamju.

**SCENE FOUR: PUYANGA AND BAMJU AT A CAFE**

**61. SFX: CUTLERY AND CUPS AS WHEN PEOPLE HAVE TEA/COFFEE**

**62. BAMJU:** Bosi, kwanza, nakushukuru kwa kuharakisha kuachiliwa kwangu niliposhikwa. Yule InspektaTino… alini --

**63. PUYANGA:** Tino si shida yetu. Sikiliza. Kuna meli mpya karibu kutia nanga. Nataka watu waaminifu wanaoweza kueneza mzigo bila kujulikana. Unafahamu kuwa yeyote asijuwe kazi hiyo ni ya nani.

**64. BAMJU:** bila shaka, mkubwa. Nafahamu vijana wawili waliokuwa wakinunua”majani” kutoka kwangu.

**65. PUYANGA:** **(whisper)** Hii ni zaidi ya bangi, Bamju. Nakuahidi kuwa huo mzigo ukiuzika tutasahau umasikini..

**66. BAMJU:** Bila shaka, Bila shaka. Mimi niko ndani, mkubwa. Watu wamechoka na kwekwe za kawaida, tumbaku, mairungi na pombe. Ni wakati tuwe na mabadiliko!

**67. SFX: MOBILE PHONE RINGS.**

**68. PUYANGA:** Ndio, haloo. Puyanga hapa... Aha, imewasili? **(Pause)** Vyema. Hakikisha kwa gharama yeyote mzigo umetoka bandarini. Sijali utawahonga senti ngapi – huo mzigo nautaka nje ya bandari leo. Kwaheri.

69. **BAMJU:** Ehm, sasa...

70. **PUYANGA:** Bamju, tuwasiliane ukiwapata hao wafanyikazi. Kumbuka, mke wangu ni afisa wa polisi. Nataka usiri wa hali ya juu. Sitaki nihuishwe na chochote...

71. **MSIMULIZI:** Puyanga alimaliza mkutano wake na kuondoka haraka. Kwengineko, Katika kituo cha polisi, Inspekta Tino anamueleza bosi wake, Beri, kuhusu mshukiwa wa hivi punde aliyemkamata.

**SCENE FIVE: AT THE POLICE STATION**

**72. INSP. TINO:** Nilimshika nje ya kilabu 2000. Alikuwa mlevi chakari.

**73. BERI:** Huyu si mdogo sana, Inspekta Tino?

**74. INSP. TINO:** Eti mdogo? Mbona alipatikana kilabu?

**75. BERI:** Kijana, unaitwa nani? Unajuwa hapa ni wapi?

**76. JABALI:** **(with hangover)** Aaah, Kichwa changu! Naomba dawa za maumivu. Tafadhali.

**OUTRO:**

Huku Jabali akiomba dawa ili kutuliza kichwa na maumivu ya usiku uliopita, tunakamilisha kipindi cha tatu cha mchezo huu kuhusu ubadirifu wa mihadarati na vileo. Usikose kujiunga nasi tena, ili upate kujua hadithi hii itatufikisha wapi. Na ukipenda kusikilizia tena kipindi hiki, tembelea tovuti zetu www.dw.de/lbe Hadi wakati mwengine – Jiepushe na mihadarati.